

AHADI ZA SERIKALI BUNGENI KUHUSU ELIMU

2016/2017

hakielimu

July 2016

AHADI ZA SERIKALI BUNGENI KUHUSU ELIMU 2016/2017

July 2016

Utangulizi

Pamoja na kuwa nchi yetu imepita katika awamu 5 za utawala wa kisiasa bado changamoto katika sekta ya elimu ni nyingi. Hali ya watoto kutojua kusoma na kuandika nchini,matokeo yasiyoridhisha katika mitihani ya darasa la saba na kidato cha nne na walimu kukosa hamasa ya ufundishaji, ni baadhiya ishara za kutokuwa na mazingira bora ya utoaji wa elimu nchini na kutotimizwa kwa wakati kwa baadhi ya ahadi za serikali katika elimu.

Ripoti ya UWEZO, 2015, inaonesha kuwa baadhi ya watoto wa darasa la saba hawawezi kufanya majaribio ya darasa la Pili na wanafunzi wanne kati ya kumi (44%) hawawezi kusoma hadithi ya Kiingereza ya kiwango cha darasa la pili.

Kwa upande wa matokeo ya mitihani, jumla ya watahiniwa 518,034 kati ya 763,602 walifaulu mtihani wa darasa la saba mwaka 2015 sawa na asilimia 67.84, ambapo kati yao wasichana walifaulu kwa asilimia 64.60 na wavulana asilimia 71.58. Hii inamaanisha kuwa asilimia 32.16 walifeli mtihani huo na hivyo kutopata nafasi ya kuendelea na masomo ya sekondari. Kwa kidato cha nne, ufaulu kwa mwaka 2015 ulikuwa asilimia 67.9 na ambao umeshuka toka asilimia 68.3 kwa matokeo ya mwaka 2014. Matokeo haya bado si mazuri kwani kundi kubwa la watahiniwa bado wanafeli mtihani.Tafsiri rahisi ya ufaulu huu ni kuwa kila kati ya wanafunzi 100, zaidi ya wanafunzi 32 walipata daraja sifuri.

Ripoti ya Benki ya Dunia kwa nchi ya Tanzania kuhusu Viashiria vya Utoaji wa Huduma-Elimu 2016, inaonesha kuwa kwa wastani, asilimia 14 ya walimu waligundulika kutokuwepo shuleni wakati walipaswa kuwepo.Utoro kutoka darasani ulikuwa juu zaidi ambapo asilimia37 ya walimu waliokuwepo shuleni, hawakuwepo darasani wakifundisha. Kuna uwezekano mkubwa kwamba utoro wa walimu darasani ni suala la uongozi wa shule na menejimenti, kwa sababu walimu wengi, walikuwepo shuleni. Baadhi ya sababu zinazochangia hali hii ni walimu kukosa hamasa ya kazi kutokana na kutolipwa stahiki zao kwa wakati, mishahara isiyokidhi mahitaji, mazingira magumu ya kufundishia kutokana na uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Ripoti ya UWEZO, 2015 inaonesha kuwa uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi kwa wanafunzi wa darasa la Pili ulikuwa 1:8,yaani wanafunzi 8 wanatumia kitabu 1 cha kusoma. Pia wasichana 125 wanatumia tundu 1 la choo, huku wavulana 130 wakitumia tundu1 la choo.Uwiano unaopendekezwa na wizara ya elimu ni 1:20 kwa wasichana na 1: 25 kwa wavulana.

Hivyo ufuatiliaji wa ahadi za serikali katika kuboresha elimu utaharakisha utekelezaji wa ahadi mbalimbali za serikali ili kutatua changamoto zilizoainishwa hapo juu na nyinginezona kuweka mazingira mazuri ya utoaji elimu nchini.Pia mipango mingi ya maendeleo ya taifa itawezeshwa kwa kuwa na rasilimali watu wenye ujuzi na elimu bora.

Shirika la HakiElimu limekuwa likifuatilia ahadi mbalimbali za serikali katika elimu kwa lengo la kuikumbusha serikali kutimiza ahadi zake kwa wananchi katika elimu na hivyo kutekeleza kwa vitendo dhana ya utawala bora na uwajibikaji katika serikali. Hivyo wananchi watakapofuatilia utekelezaji wa ahadi za serikali watakuwa wanatimiza wajibu wao wa kikatiba[1] kwa kuikumbusha serikali kutimiza wajibu wake.

Chapisho hili ni nyenzo ya kumsaidia mwananchi kufuatilia ahadi hizo. Pia chapisho hili litamsaidia mwananchi kujenga uelewa wa masuala mbalimbali yanayohusu elimu na yanayojadiliwa bungeni na kutolewa ahadi za utekelezaji. Wananchi hawana budi kufuatilia ahadi zinazotolewa na serikali bungeni na kuhakikisha kuwa zinatekelezwa ili kuboresha mazingira ya utoaji elimu nchini.

Toleo hili ni mkusanyiko wa ahadi za serikali katika sekta ya elimu zilizotolewa bungeni kufuatia mikutano

1 Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania (1977) Ibara 8(1) imetamka bayana kuwa wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na kuwa serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi.

mbalimbaliya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia Novemba 2015 hadi June 2016. Utekelezaji wa ahadi hizi unatarajiwa kufanyika katika mwaka wa fedha wa serikali 2016/2017.

Ajira kwa walimu

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mh. Selemani Said Jaffo alieleza Bungeni tarehe 03 Mei, 2016 kuwa;

Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imepanga kuajiri walimu 35,411 waliohitimu kuanzia mwaka 2013/2014 na miaka ya nyuma na kuwa sehemu ya walimu hao watapangwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Ileje. Mahitaji ya walimu wa shule za msingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ileje ni 819, waliopo sasa ni walimu 567 na upungufu ni 252. Kwa upande wa shule za sekondari mahitaji ya Walimu wa sayansi na hisabati ni 156, waliopo ni 61 na upungufu ni 95. Hata hivyo, wilaya hiyo ina zaidi ya walimu wa masomo ya sanaa 105.

Naibu Waziri huyo alikuwa akijibu swali lililoulizwa na Mh.Janet Z. Mbene mbunge wa Ileje CCM aliyetaka kujua kama Serikali iko tayari kujaza pengo la walimu liliko hivi sasa.

Madai ya walimu

Naibu Waziri wa Tamisemi, Utumishi na Utawala Bora, Selemani Said Jaffo, alieleza bungeni April 22, 2016 kwamba;

Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kukusanya madeni mapya ya walimu ambapo hadi tarehe 19 Aprili, 2016 madeni yasiyo ya mishahara yanafikia kiasi cha shilingi bilioni 17.5 kwa shule za msingi na sekondari wakati madeni ya mishahara yakifikia shilingi bilioni 49.8. Madeni haya yatafanyiwa uhakiki na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kisha kuwasilishwa Hazina ili yalipwe. Vilevile Mh. Selemani Said Jaffo alikiri kwamba madeni haya hata yakilipwa lazima yataendelea kuwapo kwasababu kila siku walimu wanahama na kila siku walimu wanaenda likizo. Jambo la msingi ni kwamba madeni yanapojitokeza, watu sasa wanapaswa kulipwa haki zao wanazostahili mara moja.

Serikali imeendelea kulipa madeni yasiyo ya mishahara na mishahara kwa walimu walioko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kila yanapojitokeza na kuhakikiwa. Aidha, mwezi Oktoba, 2015 Serikali ililipa madeni ya walimu yanayofikia shilingi bilioni 20.125 na mwezi Februari, 2016 imelipa jumla ya shilingi bilioni 1.17 ya madeni ya walimu nchini. Katika fedha za madai ya walimu zilizolipwa Oktoba, 2015 Mkoa wa Arusha ulipelekewa jumla ya shilingi milioni 504.6 ambapo kati ya hizo Halmashauri ya Wilaya ya Meru ilipokea jumla ya shilingi milioni 27.6 ambazo zilitumika kuwalipa walimu 716.



Naibu Waziri wa Tamisemi, Utumishi na Utawala Bora,Mh. Selemani Said Jaffo, alikuwa akijibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum aliyetaka kujua kuhusu suala la madai ya walimu nchini limekuwa ni tatizo sugu hususan kwa walimu wa shule za msingi na sekondari. Je, Serikali imechukua hatua gani ili kumaliza tatizo hilo?

Nyumba za walimu

Naibu Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora) Selemani Said Jaffo alisema bungeni January 27, 2016 kuwa;

Kwa upande wa Shule za Msingi, Serikali katika mwaka wa fedha 2015/2016 imetenga shilingi milioni 100 kutokana na mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa nyumba tano na shilingi milioni 127 zimetengwa kupitia ruzuku ya maendeleo (CDG) kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa nyumba sita za walimu katika wilaya ya Magu. Mahitaji ya nyumba za walimu wa Shule za Msingi katika Halmashauri ya Magu ni 1,447, zilizopo ni nyumba 284 hivyo kuwa na upungufu wa nyumba 1,183. Aidha, shule za sekondari zina mahitaji ya nyumba 396, zilizopo ni nyumba 53 na upungufu ni nyumba 343.

Mh. Selemani Said Jaffo alikuwa akijibu swali la Mh. Kiswaga Boniventura Destery, Mbunge wa Magu aliyetaka kujua Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za walimu.

Vipaumbele kwa wanafunzi wenye Ulemavu

Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mh. George Simbachawene alieleza bungeni June 23, 2016 kuwa katika bajeti ya mwaka Serikali imetenga takriban shilingi bilioni 16.633 kwa ajili ya kuzihudumia shule za watoto wenye mahitaji maalumu (wenye ulemavu). Waziri alieleza kuwa kuna shule karibu 28 kwa ajili wa watu wenye Ualibino; shule karibu 92 kwa ajili ya watu wasioona, na shule 137 kwa ajili vijana wasio na uwezo wa kusikia vizuri kwa maana ya viziwi.Aidha, kuna shule 18 kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa viungo, na shule 286 kwa ajili ya ulemavu wa akili na shule tisa kwa walemavu wa usonji.

Katika utaratibu wa sasa Serikali, inasaidia wale wanaoanza kuanzia chekechea, shule za msingi na kidato cha kwanza hadi cha nne. Kwa kidato cha tano na cha sita, utaratibu huu mara nyingi hufanywa chini ya Wakuu wa Wilaya ambao hushirikiana na Halmashauri katika kuwabaini wale ambao hawana uwezo na kuweka utaratibu wa kuwasaidia.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa George Simbachawene alikuwa akijibu swali lilioulizwa na Mh. Amina S. Mollel Mbunge wa Viti Maalum, (Kwa niaba yaMh. Dkt. Elly Marco Macha, Mbunge wa Viti Maalum) aliyetaka kujua kama serikali iko tayari kutoa elimu bure kwa wanafunzi wenye ulemavu kwa ngazi ya kidato cha tano na sita na itaweka utaratibu mzuri wa usafiri na huduma nyingine muhimu za kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu kupata elimu katika shule wanazopangiwa.

Elimu kwa watoto wenye mahitaji maalumu



Tarehe 27, Mei 2016 bungeni, Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi mh. Profesa Joyce Ndalichako aliwahakikishia waheshimiwa wabunge kwamba;

Elimu maalum itakuwa ni kipaumbele na wizara yake itahakikisha inanunua vifaa. Pia alieleza kuwa tayari kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya elimu maalum na ni fedha nyingi takribani bilioni 5. Lengo likiwa ni kutaka kuhakikisha zile kero za msingi katika elimu maalum zinaondoka. “Kwa hiyo

nirudie kuwahakikishia kwamba umuhimu wa elimu maalum tunautambua na katika bajeti yetu tumezingatia. Tumeweka fedha za kutosha na tutaendelea kuimarisha kadri uwezo wa kifedha unavyojitokeza" alisema. Profesa Ndalichako.

Ujenzi wavyuo vya ufundi VETA

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Mh. Eng.Stella Manyanya alisema Bungeni April 20, 2016 kuwa;

Ujenzi wa Chuo cha VETA cha Mkoa wa Kagera unategemea kuanza baada ya hatua za maandalizi ya msingi zitakapokamilika. Serikali kwa sasa imeshalipa kiasi cha shilingi 4,779,896 kwa ajili ya kupata Hati miliki kwa eneo lenye hekta 40.9 lililopo katika Kijiji cha Burugo, Kata ya Nyakato ambapo chuo kitajengwa. Aidha, uchambuzi wa stadi zitakazofundishwa katika Chuo hicho umekamilika. Serikali pia inaendelea kuandaa michoro kwa ajili ya majengo na miundombinu ya chuo, kuandaa mitaala kulingana na stadi zilizotambuliwa, kuandaa mipango ya ukarabati wa miundombinu hasa kilometa nne mpaka tano za barabara kutoka barabara kuu na kuhakikisha maji na umeme vinapatikana katika eneo hilo.

Aidha, Serikali inaendelea na mazungumzo na Serikali ya Watu wa China kuhusiana na ufadhili wa ujenzi wa Chuo hicho. Serikali inategemea kukamilisha ujenzi wa Chuo cha VETA cha Mkoa wa Kagera kutegemeana na upatikanaji wa Fedha na juhudi mbalimbali ikiwemo ushirikishwaji wa wafadhili wa ndani na nje ya nchi kama sehemu ya kuchangia juhudi za Serikali.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Mh. Eng. Stella Manyanya alikuwa akijibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini,aliyetaka kujua ni lini ujenzi wa Chuo cha VETA cha Mkoa wa Kagera utaanza na kukamilika.

Pia, Naibu Waziri Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi Mh. Eng. Stella Manyanya alieleza bungeni Februari 1, 2016 kuwa;Wizara yake imedhamiria kuanza kujenga vyuo vya VETA katika Wilaya zote ambazo hazina kabisa chuo chochote cha Ufundi au VETA kwa ujumla. Lakini kwa sababu ya bajeti ambayo kimsingi inahitajika katika maeneo mengi siyo rahisi kuvijenga vyuo vyote kwa siku moja.

Naibu Waziri huyo alikuwa akijibu swali liloulizwa na Mheshimiwa Mwambalaswa Mbunge wa Lupa (CCM) alieuliza kuwa serikali mwaka juzi ilitangaza kwamba itaweka vyuo vya VETA kwenye wilaya zote nchini lakini itaanza na wilaya 10 ambapo Wilaya ya Chunya ambayo imegawanyika katika wilaya mbili za Chunya na Songwe ni mojawapo. Hivyo ni bora wilaya zote mbili zikapata chuo cha VETA.

Uboreshaji wa vyuo vya VETA nchini

Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Profesa Joyce Ndalichako, alieleza bungeni Juni 29, 2016 kuwa:

Serikali itafanya mapitio ya uendeshaji wa mafunzo ya ufundi stadi nchini, kwani Wizara ya Elimu imeona kuna umuhimu wa kufanya tathmini ya mafunzo ya ufundi stadi yanayotolewa katika vyuo vyote nchini kwa lengo la kuangalia upya aina ya mafunzo yanayotolewa, na teknolojia inayotumika.Zoezi hilo litakuwa agenda namba moja baada tu ya kufunga Bunge (Bunge la bajeti 2016/2017) naitafanyika tathmini kwa nchi nzima. Profesa Joyce Ndalichako alieleza kuwa amekuwa akiwasikiliza sana waheshimiwa wabunge na michango yao mizuri na maswali yao kuhusiana na VETA na kuwa wamekuwa pia wanahoji kuhusiana na teknolojia. Kwa mfano, baadhi ya vyuo vya ufundi vinaendelea kutumia labda cherehani za miguu, wakati zimepitwa

na wakati kwa hiyo hiyo ni tathmini ya ujumla ambayo itahusisha nchi nzima. Baada ya hapo hatua mahsusi zitachukuliwa kuhakikisha kwamba VETA inatoa mafunzo ya kisasa yanayoendana na mahitaji ya sasa hivi ya viwanda vinavyotarajiwa kuanzishwa.

Profesa Ndalichako alikuwa akijibu swali lililoulizwa na Mh. Mashimba M. Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi (CCM) aliyeuliza; kwa kuwa kuna chuo kizuri cha VETA pale Maswa Mjini na kwa kuwa pia, kuna Chuo cha Maendeleo ya Jamii Malampaka, wakati huu ambapo matayarisho ya kujenga Chuo cha VETA cha Mkoa yanaendelea, je, Serikali ina mpango gani wa kuviboresha vyuo hivi viwili ili viweze kuanza kuchukua vijana wakati mpango wa kujenga Chuo cha VETA mkoani unaendelea?

Hitaji la Chuo cha Ufundi VETA-Simiyu

Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi Mh. Profesa Joyce Ndalichako alieleza bungeni Juni 29, 2016 kuwa:

Serikali ya Mkoa wa Simiyu tayari imeshatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha VETA cha Mkoa wa Simiyu, katika bajeti ambayo waheshimiwa wabunge waliipitisha ya Wizara, na kuwa kiasi cha shilingi bilioni 4 kimetengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya ujenzi huo. Maandalizi ya awali ikiwemo kumpata mshauri elekezi, uandaaji wa michoro pamoja na makadirio ya ujenzi yaani Bills of Quantities (BOQ) na kumpata Mkandarasi yanatarajiwa kukamilika ifikapoNovemba, 2016.Ujenzi unatarajiwa kuanza rasmi mwezi Januari, 2017. Lengo la ujenzi wa Chuo cha VETA cha Mkoa wa Simiyu ni kutoa mafunzo ya ufundi stadi na huduma kwa vijana wanaohitimu elimu ya msingi na sekondari katika Wilaya zote za Mkoa wa Simiyu ili waweze kupata elimu ya ufundi na hivyo kuwawezesha kujiajiri.

Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Profesa Joyce Ndalichako alikuwa akijibu swali lililoulizwa na Mh. Mashimba M. Ndakimbunge wa Maswa Magharibi CCM kwa niaba ya Mh. Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Viti Maalum aliyeuliza; Kwa kuwa Mkoa wa Simiyu hauna Chuo cha Ufundi (VETA) na kuwa vijana wengi wanahitimu elimu ya msingi na sekondari: Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga chuo cha ufundi ili vijana hao waweze kupata elimu ya ufundi na kuweza kujiajiri?

Ukarabati wa vyuo vya Maendeleo ya wananchi

Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi Mh. Profesa Joyce Ndalichako alieleza bungeni Mei 26, 2016 kuwa;

Katika mwaka 2016/17, Wizara yake kwa kutumia fedha zilizokuwa zimetengwa chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itaanza ukarabati wa vyuo vya Maendeleo ya wananchi Ilula, Newala na Kilosa. Aidha, itajenga vyoo katika vyuo vya Buhangija, Bariadi na Kisarawe. Vilevile itaunganisha umeme katika vyuo vya Mwanhala, Malya, Rubondo, Ulembwe, Munguri na Msingi. Wizara pia itashughulikia upatikanaji wa hatimiliki wa vyuo vya Kilwa Masoko, Chisalu, Kisarawe, Chilala, Arnautoglu, Musoma, Mwanva, Ikwiriri, Msingi na Ifakara.

Ada elekezi kwa shule binafsi

Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi Profesa Joyce Ndalichako alieleza bungeni Januari 28, 2016 kuwa;

Suala la ada kubwa zinazotozwa na shule binafsi linafanyiwa kazi na wizara yake na kwamba wizara itakuja na ada elekezi baada ya kufanyiwa kazi kwa kina.Waziri Ndalichako alisisitiza kuwa suala la ada elekezi linahitaji kufanyiwa kazi kwa kina na kuangalia vizuri kwa sababu shule ziko katika makundi mbalimbali.

"Wizara yangu lazima iliangalie hili jambo kwa umakini mkubwa sana. Tutaangalia mpaka mishahara wanayolipwa walimu. Kuna baadhi ya shule zinawaonea walimu zinawapa mishahara kidogo. Kwa hiyo, naomba watanzania tuwe na subira, Wizara yangu inalifanyia kazi hili jambo, lakini siyo jambo ambalo linahitaji kufanya kazi kwa haraka. Tutakapokuwa tayari, tutakuja kuwapa majibu," alisema, Profesa Ndalichako.

Elimu bila malipo

Naibu Waziri waTAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora Mh. Selemani Said Jaffo alieleza bungeni tarehe 29 Januari, 2016 kuwa;

Kuanzia Januari, 2016 Serikali imeamua kuwa itawalipia ada na michango mbalimbali iliyokuwa inagharimiwa na wazazi na walezi, wanafunzi wote walioandikishwa darasa la kwanza na kidato cha kwanza pamoja na wale wanaoendelea na shule.

Kwa kuanzia Serikali imetenga shilingi bilioni 131.4 ikiwa ni fedha za ruzuku ya uendeshaji wa shule, chakula, mitihani na fidia ya ada. Fedha hizo zitapelekwa moja kwa moja shuleni kutoka Hazina kwa wastani wa shilingi bilioni 18.77 kila mwezi. Fedha hizo zinahusisha shilingi 10,000/= kwa wanafunzi wa shule ya msingi kwa mwaka, shilingi 25,000/= kwa mwanafunzi wa sekondari kwa mwaka, shilingi 1,500/= kwa kila mwanafunzi kwa shule za msingi na sekondari kwa ajili ya chakula, fidia ya ada ya shilingi 20,000/= kwa wanafunzi wa kutwa na shilingi 70,000/= kwa wanafunzi wa bweni kidato cha kwanza hadi cha nne kwa mwaka.Hapo awali fedha za uendeshaji wa elimu (capitation) zikiwemo shilingi 10,000/= kwa wanafunzi wa shule ya msingi na shilingi 25,000/= kwa wanafunzi wa sekondari zilikuwa hazipelekwi kwa ukamilifu.

Naibu Waziri wa TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora Mh. Selemani Said Jaffo alikuwa akijibu swali lililoulizwa na Mh. Tunza I. Malapo: mbunge wa viti maalumu Chadema aliyetaka kujua namna ambavyo serikali imejipanga kutekeleza Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 kwa kutoa elimu bure bila kuathiri ubora wa elimu.

Utengenezaji wa madawati na utekelezaji elimu bila malipo

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi Mh. Eng. Stella Manyanya alieleza bungeni January 26, 2016 kuwa;

Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji itahakikisha inatenga fedha kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa madawati. Sambamba na hilo, wananchi na wadau wengine wa elimu wataendelea kusaidia kuchangia katika upatikanaji wa madawati kwa kadri watakavyoona inafaa. Pia alieleza kuwa Serikali imeanza utekelezaji wa utoaji wa elimu msingi bila malipo ambapo jumla ya shilingi bilioni 15.71 zimepelekwa katika Shule za Msingi na Sekondari za Umma kwa mwezi Desemba, 2015. Fedha hizi ni kwa ajili ya ruzuku ya uendeshaji shule, fidia ya ada kwa shule za sekondari za bweni na kutwa na chakula kwa wanafunzi wa bweni. Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule wamepewa Mwongozo wa matumizi ya fedha ambazo zitatumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, zikiwemo chaki, gharama za ulinzi, mitihani na chakula.

"…kwa maelezo hayo, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba hakuna Mkuu wa Shule au Mwalimu Mkuu yeyote ambaye atamrudisha mwanafunzi nyumbani kwa kutolipa michango ya mlinzi,

madawati na chaki kwa sababu, majukumu hayo ni ya Serikali. Serikali ina dhamira ya kuendelea kuboresha utekelezaji wa mpango huu kadri ya tafiti zitakavyoonesha, pamoja na maoni ya wadau mbalimbali yakiwemo ya ninyi waheshimiwa Wabunge," alisemaMh. Stella Manyanya.

Mh. Manyanya alikuwa akijibu swali liloulizwa naMh. Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda aliyetaka kujua Serikali imejipanga vipi kuhakikisha wanafunzi hawarudishwi shule kwa sababu ya michango ya mlinzi, madawati na chaki.

Ukarabati wa miundombinu ya shule



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Selemani Said Jaffoalieleza Bungeni Mei 03, 2016) kuwa; Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri ya Ileje imetengewa shilingi milioni 130.8 ili kuendelea na uboreshaji wa mindombinu ya Shule ya Sekondari ya Ngulilo. Aidha, kupitia mapato yake ya ndani Halmashauri imetenga shilingi milioni 60.0 kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za walimu, ukarabati wa vyumba vya madarasa, ujenzi wa matundu ya vyoo na matengenezo ya madawati. Jitihada hizi zinakusudiwa kuinua kiwango cha elimu inayotolewa kwa wanafunzi katika Wilaya ya Ileje. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, zilitengewa shilingi milioni 798.0 ambazo zilipokelewa kwa ajili ya ukarabati, ujenzi na umaliziaji wa miundombinu ya shule nne za Msomba, Luswisi, Itale na Bupigu.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mh. Selemani Said Jaffo, alikuwa akijibu swali lililoulizwa na Mh. Janet Z. Mbene Mbunge wa Ileje (CCM) aliyetaka kujua Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa inaboresha miundombinu yote muhimu kwa utoaji wa elimu.

Ukarabati wa shule kongwe

Tarehe Mei 26, 2016, Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi Mh. Profesa Joyce Ndalichako alieleza bungeni kuwa;

Katika mwaka 2016/17, Wizara yake imeandaa mpango wa ukarabati wa shule kongwe za sekondari nchini ambapo katika awamu ya kwanza shule 33 zitakarabatiwa. Shule hizi ni Ihungo, Ilboru, Kilakala, Mwenge, Msalato, Mzumbe, Nganza, Pugu, Same, Tabora Boys na Tabora Girls. Shule nyingine ni Azania, Jangwani, Kantalamba, Mpwapwa, Tosamaganga, Malangali, Milambo, Nangwa, Kibiti, Minaki, Ifakara, Songea Boys, Ndanda, Kigoma,



Shule ya sekondari Tosamaganga

Kibaha na Shule za Ufundi za Bwiru Boys, Ifunda, Iyunga, Moshi, Mtwara, Musoma na Tanga.
"Naomba nilihakikishie Bunge lako tukufu kuwa zile shule zitarudi katika hadhi yake, zitatoa elimu bora, zitakuwa na mazingira mazuri na watanzania watanufaika kama ambavyo sisi tumenufaika,"alisema.

Ujenzi wa mabweni ya sekondari kidato cha Tano

Tarehe 20 Juni, 2016 Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mh.Selemani Said Jaffo alilieleza Bunge kuwa;

Ili kuhakikisha shule ya Sekondari ya Bulende iliyopo katika Halmashauri ya Mji wa Nzega inapata sifa ya kuwa ya kidato cha tano Serikali imetenga shilingi milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa bweni katika bajeti ya mwaka 2016/2017. Ili shule iweze kusajiliwa kuwa ya kidato cha tano na sita inapaswa kuwa na miundombinu ya kutosha kama vyumba vya madarasa, mabweni, samani, bwalo la chakula, vyoo pamoja na uwepo wa walimu wa masomo husika.

Halmashauri inapaswa kuwasilisha maombi ya usajili wa shule katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Ufundi ambayo itatuma wataalam kukagua miundombinu ya shule kabla ya kutoa kibali. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha miundombinu ya kutosha inajengwa kwa kushirikisha nguvu za wananchi katika shule ya Sekondari ya Chief Itinginya ili kukidhi taratibu na kusajiliwa kuwa ya kidato cha tano. Pia Halmashauri imepanga kutenga bajeti katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule ya sekondari ya Chief Itinginya.

Naibu Waziri huyo alikuwa akijibu swali la Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Mbunge wa Nzega Mjini aliyetaka kujua kwa kuwa Halmashauri ya Mji wa Nzega haina shule hata moja ya kidato cha tano na sita na hivyo kuwafanya wanafunzi wengi kulazimika kwenda kusoma nje ya Mji wa Nzega, je, ni lini Serikali itajenga vyumba vya madarasa ya kidato cha tano na sita katika shule ya sekondari Chief Itinginya ili angalau kuwe na shule mbili za kidato cha tano na sita. Mbunge kwa jitihada zake amejenga vyumba viwili pamoja na bweni katika shule ya sekondari Bulende kwa ajili ya kidato cha tano na sita;

Kuinua ubora wa Elimu

Mnamo tarehe 4 Mei, 2016, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Mh. Eng.Stella Manyanya alisema bungeni kuwa, ili kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa nchini inakuwa na ubora wa hali ya juu, Serikali ya Awamu ya Tano ina mikakati mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kuimarisha na kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kujenga na kukarabati miundombinu ya shule, ikiwemo ujenzi wa vyumba vya madarasa, maabara, maktaba, vyoo, nyumba za walimu na ununuzi wa madawati.
(ii) Kuendeleza mafunzo ya walimu tarajali hususan kwa masomo ya sayansi, hisabati, lugha na elimu ya awali.
(iii) Aidha, Serikali inaendesha mafunzo kazini kwawalimu kuhusu matumizi ya stadi za TEHAMA, sayansi, hisabati na lugha ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu wa shule za msingi na sekondari.
(iv) Katika kuimarisha stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) mafunzo yanatolewa kwa walimu wa darasa la kwanza na la pili.
(v) Vile vile ili kuimarisha ufuatiliaji wa tathmini ya ubora wa elimu itolewayo, Ofisi za Udhibiti Ubora wa Shule, Kanda na Wilaya zinaendelea kuimarishwa kwa kuongeza idadi ya Wadhibiti Ubora wa Shule na vitendea kazi.

Mh. Stella Manyanya alikuwa akijibu swali lilioulizwa na Mhe. Susan A.J. Lyimo,Viti Maalumu, CHADEMA, kujua Serikali ya Awamu ya Tano ina mikakati gani ya kuinua ubora wa elimu hapa nchini kwani, mwaka 2015 HakiElimu walitoa tathmini ya utafiti wa elimu kwa kipindi cha miaka 10 ya Awamu ya Nne na kugundua ongezeko kubwa la udahili kwa ngazi zote na kuporomoka kwa ubora wa elimu nchini.

Nishati ya umeme shuleni

Tarehe 22, April 2016, Naibu Waziri wa Nishati na Madini Mh. Dkt. Medard Kalemani alieleza bungeni kuwa katika Mpango wa Awamu ya Pili ya Umeme Vijijini maeneo ya huduma za jamii ambayo yatafikishiwa huduma ya umeme katika Halmashauri ya Mbeya Vijijini ni pamoja na shule za msingi 23, na shule za sekondari 5. Mradi wa REA II unaotekelezwa katika Awamu ya Pili katika Vijiji 27 vya Halmashauri ya Mbeya, unafanywa na Mkandarasi SINOTEC na umefikia asilimia 54.33 na mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2016/2017.

Mh. Kalemani alieleza pia kuwa katika miradi yote inayotekelezwa na Serikali kupitia Mfuko wa REA Vijijini, kipaumbele kimewekwa kwenye huduma za kijamii kama vile shule, zahanati, vituo vya afya, nyumba za ibada na mashine za kusukuma maji.

Dkt. Kalemani alikuwa akijibu swali lililoulizwa naMh. Oran Manase Njenza, Mbunge wa Mbeya Vijijini aliyetaka kujua katika utekelezaji wa Mradi wa REA II Mbeya vijijini ni vijiji vingapi vya Halmashauri ya Mbeya vimo kwenye REA II na mradi utakamilika lini?Pia alitaka kujua kwanini mradi wa REA II haujalenga kupeleka umeme kwenye huduma za kijamii kama vile shule, zahanati, nyumba za ibada na vyuo?

Vifaa vya maabara kwa sekondari

Tarehe 27, Mei 2016, Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi Mh. Profesa Joyce Ndalichako alilieleza Bunge kuwa,



Jukumu la kununua vifaa vya maabara liko katika ofisi ya Rais TAMISEMI lakini Wizara yake imetenga kiasi cha shilingi bilioni 12 kwa ajili ya kununua vifaa vya maabara na tayari hizi ni katika fedha za mwaka unaokwisha. Prof. Ndalichako alieleza pia kuwa wanataka kuona kwamba wanafunzi wanajifunza Sayansi kwa vitendo na siyo kwa nadharia. Alisema shule zote ambazo zimejenga maabara na zimekamilika kabisa mpaka mwezi Februari zilikuwa shule 1,536 na kwamba hizi zote zitapata vifaa.

Pia, Waziri waNchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mh. George B. Simbachawene alieleza bungeni Mei 26, 2016 kuwa;

Katika mwaka 2016/17 Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa shule zote za sekondari zina vifaa vya maabara na vitabu vya kutosha ambapo tayari Wizara ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imetangaza zabuni ya ununuzi wa vifaa hivyo vya maabara na uchapaji wa vitabu hivyo, ambavyo vitasambazwa nchini kote. Maabara zote zilizojengwa na Halmashauri kwa kushirikiana na wananchi zitapatiwa vifaa vya maabara. Ununuzi wa vifaa hivyo vya maabara utafanyika kwa awamu tatu ambapo awamu ya mwisho inategemewa

kukamilika mwaka wa fedha 2018/19. Nia ya Serikali katika mpango huu ni kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inakidhi viwango na wanafunzi wanapatiwa zana zote muhimu katika kujifunza.

Utoaji wa Elimu ya Kompyuta Mashuleni

Naibu Waziri wa Tamisemi, Utumishi na Utawala Bora alijibu swali la Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, April 29, 2016 kama ifuatavyo:

Utoajiwa elimu ya kompyuta mashuleni umeanza kufanyika kwa baadhi ya shule zenye mazingira yanayowezesha somo hilo kufundishwa. Changamoto zilizopo ni uhaba wa walimu, ukosefu wa umeme hususani maeneo ya vijijini na uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Serikali inakabiliana na changamoto hizo kwa kupeleka umeme vijijini kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA), pamoja na kuhakikisha somo la Kompyuta linafundishwa katika Vyuo vya Ualimu ili kuwaandaa walimu watakaofundisha somo hilo mashuleni.

Kuhusu upatikanaji wa vifaa mashuleni Serikali inashirikiana na Kampuni ya Microsoft ambayo imeonesha nia ya kuwezesha upatikanaji wa vifaa hivyo. Mpango wa muda mrefu wa Serikali ni kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ufundishaji mashuleni hususani masomo ya sayansi. Kwa msaada wa Kampuni ya Microsoft serikali imeanza utekelezaji wa mpango huu kwa shule 50 katika mikoa 25. Kwa Mkoa wa Rukwa shule zilizochaguliwa ni shule ya Sekondari ya Kizwite na Mazwi. Shule hizi mbili za kila mkoa ni vituo vya mafunzo kwa walimu ili kuwajengea uwezo wa kufundisha kwa kutumia TEHAMA. Kituo cha Mazwi kinaanza kufanya kazi kuanzia Julai, 2016 ambapo kitapewa vifaa vyote muhimu vitavyohitajika katika mafunzo hayo.

Naibu Waziri huyo wa Tamisemi, Utumishi na Utawala Bora alikuwa akijibu swali liliulizwa na Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum, aliyetakakujua Serikali imeamua kutoa elimu ya kompyuta kwenye shule za sekondari nchini lakini vifaa vya kufundishia havitoshelezi na hata walimu ni wachache katika maeneo mengi ikiwemo Mkoa wa Rukwa, ambapo ni shule mbili pekee za Mazwi na Kizwite Sekondari ambazo zimeshaanzishwa.

Hitimisho

HakiElimu inaishauri serikali kutekeleza kikamilifu ahadi zake katika sekta ya elimu kwani ndio msingi wa rasilimali watu inayotegemewa katika sekta zote nchini. Uwekezaji mzuri katika rasilimali watu ndio njia pekee itakayozalisha watu wenye ujuzi na maarifa ya kuipeleka Tanzania miongoni mwa nchi zenye uchumi wa kati.

Idadi kubwa ya shule za msingi na sekondari zinakabiliwa na upungufu wa miundombinu muhimu kama madarasa na maabara pia vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama vitabu. Hivyo utekelezaji mzuri wa ahadi hizi katika sekta ya elimu utafanya ubora wa shule zetu kuongezeka na kuimarika kwa ubora wa elimu nchini. Kama wadau wa elimu tumehamasika na jitihada zinazofanywa na serikali ya Awamu ya 5 katika kuinua kiwango cha elimu nchini likiwemo la kudhibiti ubora wa elimu inayotolewa na vyuo vikuu. Hivyo tunaaamini kuwa serikali ya Awamu ya 5 itasimamia vizuri utekelezaji wa ahadi zake katika elimu na fedha iliyopangwa kwa ajili ya miradi ya elimu itafika kwa walengwa na kwa wakati. Pia matatizo na changamoto wanazokabiliana nazo walimu zikiwemo za mazingira mabovu ya kufundishia, uhaba wa nyumba za walimu na mishahara isiyokidhi mahitaji halisi yatapungua na walimu watabaki katika katika vituo vyao vya kazi na kufundisha.

Endapo Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi pamoja na wizara nyingine zitawajibika kwa ahadi walizozitoa katika elimu, uwajibikaji utaongezeka na kuwafanya viongozi kufanya kazi kwa uaminifu na kufikia maamuzi sahihi katika kusimamia utekelezaji wa ahadi za serikali katika sekta ya elimu. Pia itaharakisha ufikiaji wa mipango na malengo mbalimbali ya Taifa ikiwemo malengo ya Matokeo Makubwa Sasa katika sekta ya elimu.

Nani ana wajibu wa kufuatilia ahadi za serikali katika elimu?

- Wananchi wana haki ya kuhoji kuhusu utendaji wa serikali yao katika huduma mbalimbali za jamii kupitia wawakilishi wao ambao ni wabunge. Mbunge ndiye msimamizi mkuu wa serikali kuona kuwa inawajibika ipasavyo kwa wananchi kwa kuishauri serikali kusimamia utekelezaji wa mipango yake yote ili kuwaletea wananchi maendeleo.
- Kwa kutumia fursa waliyonayo kama kiunganishi cha wananchi na serikali wabunge hawana budi kuhoji katika vikao vya bunge hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa ahadi hizi na nyingine nyingi katika sekta ya elimu ili kuongeza uwajibikaji. Pia kuishauri wizara nini kifanyike katika miaka mitano ijayo ili kufikia malengo hayo.
- Wabunge kupitia kamati zao za bunge na vikao vya bunge waishauri ikiwezekana kuishinikiza serikali kuongeza bajeti ya elimu hasa katika miradi ya maendeleo ya elimu. Kuongezwa kwa bajeti ya elimu kutasaidia katika kuweka mazingira mazuri ya utoaji wa elimu nchini.
- Wabunge hawana budi kufuatilia taarifa za utekelezaji na tathmini ya miradi iliyopo chini ya mpango wa matokeo makubwa sasa kwa kuzingatia kiwango cha uwekezaji wa rasilimali uliofanyika.

HakiElimu enables citizens to make difference in education and democracy

P.O Box 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Tel (255 22) 2151852 / 3 • Fax (255 22) 2152449
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org